

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

PARLIAMENT OF TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

KIKAO CHA SITA

BUNGE LA TANZANIA



11 SEPTEMBER, 2018

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

KIKAO CHA SITA – TAREHE 11 SEPTEMBER, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 [*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 [*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*].

MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 [*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*].

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

68. MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MCHINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kumekuwa na raia wengi kutoka Msumbiji katika Jimbo la Mchinga hasa Vijiji vya Kilangala B,

Butamba, Mvulenzi, Kitolambwani na Kikonde ambao wamekuwa wakishiriki uchaguzi katika nchi zote mbili Tanzania na Msumbiji:-

(a) Je, raia hao ni Watanzania au wa Msumbiji;

(b) Je, Serikali imepitisha utaratibu wa uraia pacha na kuwapa watu maalum.

69. MHESHIMIWA GODBLESS JONATHAN LEMA (ARUSHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mishahara ya Taasisi za Umma hupangwa na Serikali. Utaratibu huo wa Serikali kupanga mishahara ya Watumishi wake huathiri pia upangaji na ukadiriaji mishahara katika Taasisi Binafsi:-

Je, Serikali haioni haja ya kuboresha mishahara yake na kuzielekeza Taasisi Binafsi kulipa mishahara inayoendana na hali ya maisha.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

70. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Katika Mji Mdogo wa Mbalizi kuna ardhi ya ukubwa wa zaidi ya ekari 5,000

iliyotengwa kwa ajili ya Tanganyika Packers ambayo haijaendelezwa kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita:-

- (a) Je, ni lini Serikali itawarudishia Wananchi wa Mji Mdogo wa Mbalizi eneo hilo kwa lengo la kuliendeleza kwa kubadili matumizi kutokana na kukua kwa kasi kubwa kwa Mji wa Mbalizi;
- (b) Pamoja na kubadili matumizi ya ardhi hiyo, Je, Serikali ina mpango gani kwa Wananchi wanaotumia ardhi hiyo hasa ikizingatiwa kuwa wengi wao hawakupewa fidia yoyote.

71. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Nkwenda I ni Kata ya kibashara yenye Wakazi wengi na Rais Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa Kampeni katika Uchaguzi Mkuu wa 2015 aliahidi kujenga barabara kwa kiwango cha lami:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kujenga kilometra kadhaa za lami ili kupunguza adha wanazopata Wafanyabiashara hao.

72. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Halmashauri ya Mji wa Tarime imebahatika kuwa na Uwanja wa Ndege wa Magena ambao umekuwa ukitumika na Watalii wanaokwenda Mbuga ya Serengeti, Viongozi mbalimbali na hata Mgodi wa ACCASIA, Miundombinu ya Uwanja pamoja na barabara zake ni mbovu sana:-

- (a) Je, ni lini Serikali itapanua Uwanja huu na kurekebisha miundombinu yake ili Ndege nyingi ziweze kutua kwa ajili ya Watalii waendao Serengeti;
- (b) Je, ni kwa nini Serikali haijajenga jengo la Uhamiaji katika Uwanja huo ili kutoa urahisi wa Watalii wanaotumia uwanja huo.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

73. MHESHIMIWA OSCAR RWEGASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni lini Jeshi la Kujenga Taifa litakuja na mkakati wa kuwa na miradi itakayounganishwa na jitihada

za Vijana wasiokuwa na ajira Wilayani Biharamulo na kwingineko kwa namna isiyohitaji uwekezaji mkubwa wa kujenga Kambi za Kijeshi.

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

74. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA (TUMBATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuandaa Rasilimali Watu ili kufanikisha azma nzuri ya Uchumi wa Viwanda kwa nchi.

75. MHESHIMIWA ALLAN JOSEPH KIULA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Je, ni lini Serikali itajenga soko la Kimataifa katika Kata ya Mwangenza kwa ajili ya kuweka katika madaraja Vitunguu vinavyolimwa maeneo hayo ili kuvisafirisha katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

76. MHESHIMIWA SUZANA CHOGISASI MGONUKULIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali inamhudumia Faru Fausta kwa gharama ya Shilingi milioni 64 kwa Mwezi. Faru huyo hazalishi kutokana na kuwa mzee sana, lakini Serikali hiyo ~~hiyo~~ haiwezi kumhudumia Mwananchi aliyezeeka ambaye hawezi kufanya shughuli zozote za kujikimu kimaisha na hana mtu wa kumsaidia:-

• Je, ni kipi kilicho muhimu zaidi kwa Serikali kati ya Faru Fausta au Mwananchi mzee asiyeweza kufanya lolote na hana wa kumsaidia.

WIZARA YA KILIMO:

77. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa kurekebisha Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2004 ambayo imepitwa na wakati.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

78. MHESHIMIWA MWANTAKAJE HAJI JUMA (BUBUBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha ma Mipango:- Zipo Benki zinazotoa mikopo ya Kilimo hususan Benki ya Kilimo Tanzania:-

Je, kwa upande wa Zanzibar ni Wananchi wangapi wanaofaidika na mikopo ya Kilimo.

WIZARA YA ELINU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

79. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Kumekuwepo na mkanganyiko wa Elimu ya Msingi nchini ambapo kuna Sera inasema Elimu ya Msingi ni kuanzia Darasa la Kwanza mpaka Darala la Saba na nyingine inasema Elimu ya Msingi ya Mtanzania ni kuanzia Darasa la Kwanza mpaka la Kumi na Mbili:-

Je, Serikali inasema nini juu ya suala hilo.

80. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

- (a) Je, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, ni Vijana/Wanafunzi wangapi walikosa vigezo vya kupata mkopo wa Elimu ya Juu;
- (b) Je, Serikali inatumia utaratibu gani kuwatambua Wanafunzi wanaotoka katika familia maskini katika utaratibu wa utoaji mikopo ya Elimu ya Juu.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

81. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Kivuko cha Mv Mafanikio kitalala Upande wa Msangamkuu ili kuwezesha dharura

zinazojitokeza za Wagonjwa hasa Akina mama Wajawazito kuhudumiwa wakati wa usiku.

82. MHESHIMIWA MARTIN ALEXANDER MTONDA MSUHA (MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ujenzi wa barabara ya Mbanga hadi Mbambabay kwa kiwango cha lami unatarajiwa kukamilika lini.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

**(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na
Kusomwa Mara ya Tatu)**

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 [The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018].

**DODOMA
11 SEPTEMBA, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**